TGNP



# MAONI YA MTANDAO WA JINSIA TANZANIA (TGNP) NA WASHIKA WAKE,

KUHUSU **MISWADA YA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023; SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023; PAMOJA NA SHERIA YA MASUALA YA VYAMA VYA SIASA, 2023.**

Yamewasilishwa bungeni katika kamati ya bunge ya utawala, katiba na sheria mnamo tarehe 09 januari 2024.

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya kwanza Kifungu cha 3: **Tafsiri za Maneno** | Tafsiri za maneno | Tafsiri za maneno au dhana za Kijinsia zilizotumika kwenye muswada hazijawekwa katika kifungu cha 3 cha Muswada. | Kuongezea baadhi ya maneno na tafsiri zake mfano: Jinsi, Jinsia, Usawa wa kijinsia, Rushwa ya ngono, Ubaguzi, na sera jumuishi. | Kuepusha matumizi kinzani ya maneno hayo. |
| Sura ya tatu Kifungu cha 32 **Uteuzi wa wagombea wa Kiti cha Rais na Makamu wa Rais** | **Kifungu cha 32 –** 'Kila unapofanyika uchaguzi wa Rais, kila chama cha siasa kilichosajiliwa na kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume jina la mgombea wa kiti cha Rais na jina la mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais wa chama hicho'. | Msingi wa usawa haukubainishwa kwenye uteuzi wa Rais na Makamu wake. Msingi huu usipobainishwa wazi katika kifungu hiki nchi itaweza kutumbukia kwenye changamoto kwenye nafasi za maamuzi katika ngazi za juu kabisa ya kuhodhiwa na jinsi moja. | **Tunapendekeza kifungu hiki cha 32 kisomeke kama ifuatavyo;**<br>"Kila unapofanyika uchaguzi wa Rais, kila chama cha siasa kilichosajiliwa na kinachokusudia kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume jina la mgombea wa kiti cha Rais na jina la mgombea wa nafasi ya Makamu wa Rais wa chama hicho kwa kuzingatia uwiano wa jinsi na Muungano'<br><br>**Nafasi ya Mgombea urais ikiwa ni mwanamke, nafasi ya makamu wa Rais iwe ni mwanaume kwa vyama vyote vya siasa.** | Hii itasaidia kuleta usawa wa Kijinsia katika ngazi za juu za uongozi ulio endelevu kwa vyama vyote vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi. |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Nne na Tano Vifungu 51(1) na 63 (1): **Uchaguzi wa wabunge na Madiwani: suala la gharama za dhamana** | 51.- (1) - Wakati wa kurudisha fomu ya uteuzi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 50, mgombea ataweka dhamana kwa msimamizi wa uchaguzi ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa.<br><br>63 (1) – Kama hapo juu | Gharama zinazobainishwa kuhusu dhamana zimekuwa na zinaweza kuendelea kuwa kikwazo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wengi wenye nia na uwezo wa uongozi kuonesha nia ya kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. | Tunapendekeza vifungu vya 51 (1) na 63 (1) vifute dhana ya dhamana ya fedha kwa wagombea wa ubunge na udiwani katika kurejesha fomu ya uteuzi. | Dhamana ya fedha inabinya haki ya mtu kugombea hasa wanawake, vijana, watu wenye Ulemavu na wanaume wa kipato duni. |
| Sura ya Nne Kifungu cha 54(2) kinaruhusu **Mgombea pekee** | (2) Mgombea wa nafasi ya ubunge aliyetangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atapigiwa kura ya ndio au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Mbunge endapo atapata kura nyingi za ndiyo kati ya kura zote halali zilizopigwa. | Kinatoa mwanya kwa mgombea ambaye hakubaliki na wananchi wa jimbo au kata yake kuweza kupita kwa kura za idadi ndogo. | **Tunapendekeza kifungu hiki kiboreshwe na kisomeke:**<br><br>'(2) Mgombea wa nafasi ya ubunge aliyetangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atapigiwa kura ya ndio au hapana na atakuwa amechaguliwa kihalali kuwa Mbunge endapo atapata kura za **NDIYO kwa zaidi ya nusu ya kura zote halali zilizopigwa'.** | Ili kuepusha rushwa ya wenye fedha kushawishi wagombea wengine hasa wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na wanaume wa kipato duni wasigombee. |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Nne, Sehemu ya Tatu : **Kifungu kipya cha 62 (2) Uteuzi wa wagombea udiwani** | | Ii kuleta usawa wa jinsia katika kugombea nafasi za udiwani vyama vya siasa vilazimike kuzingatia uwiano wa kijinsi, ujumuishi wa vijana hususani wasichana na watu wenye ulemavu katika uteuzi. | Kuongezwe kifungu kipya cha 62; (2) na kifungu cha 62. (2) kuwe namba 62 (3). Kifungu kipya cha 62 (2) kisomeke kama ifuatavyo: uteuzi utazingatia usawa wa kijinsia kwenye kuviagiza vyama vya siasa kuteua wagombea wawili mmoja mwanamke, na mwingine mwanaume. | Kuongeza ushiriki wa wanawake katika uchaguzi na kusaidia utekelezaji wa kifungu 10C kilichoongezwa kwenye sheria ya vyama vya siasa. |
| Sura ya Nne, Sehemu ya Tatu : **Kifungu kinachotakiwa kubadilika kiwe cha 62 (3) [a, b]: Uteuzi wa wagombea udiwani** | 62 (3) - Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na watu wanaomdhamini mgombea huyo na itakuwa na taarifa zifuatazo :<br>(a) jina, anwani na kazi ya mgombea ; (b) majina na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupiga kura | Kifungu kinakosa maswali yahusuyo takwimu zenye mnyambuliko wa Kijinsia ambazo zitasaidia katika kutoa taarifa sahihi zinazohusu ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika uchaguzi. | Tunapendekeza kifungu kibadilike namba kuwa 62(3) kutokana na pendekezo la kuingiza kifungu kipya cha 62(2)<br><br>Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke :<br>(2) Uteuzi utafanyika kwa kutumia fomu itakayoainishwa ambayo itazingatia **Jinsia na matumizi ya watu wenye mahitaji maalumu, itakayosainiwa na mgombea na watu wanaomdhamini mgombea huyo na itakuwa na taarifa zifuatazo:**<br><br>**(a)** jina, **Jinsi, tarehe ya kuzaliwa, hali ya ulemavu** anwani na kazi ya mgombea;<br><br>**(b)** majina, **Jinsi, tarehe za kuzaliwa, hali ya ulemavu** na anwani za wadhamini na namba za kadi zao za kupiga kura. | Itasaidia kuzalisha takwimu zenye mchanganuo wa uwiano wa Kijinsia. |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu 63 (1) – **Uteuzi wa Mgombea** | 63.- (1) - mujibu wa masharti ya kifungu cha 62, mgombea ataweka dhamana kwa msimamizi wa uchaguzi ya kiasi cha fedha kitakachoainishwa. | Gharama zinazobainishwa kuhusu dhamana zimekuwa na zinaweza kuendelea kuwa kikwazo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wengi wenye nia na uwezo wa uongozi kuonesha nia ya kushiriki katika mchakato wa uchaguzi. | Tunapendekeza vifungu vya 63 (1) na kifute **dhana ya dhamana ya fedha kwa wagombea** wa ubunge na udiwani katika kurejesha fomu ya uteuzi. | **Dhamana ya fedha inabinya haki ya mtu kugombea hasa wanawake, vijana, watu wenye Ulemavu na wanaume wa kipato duni.** |
| Sura ya Sita Sehemu ya Sita (112) (1) **Uteuzi wa wabunge wa viti maalum** | Kifungu 112.- (1)(2) (3) (4) - Kutakuwa na Wabunge wanawake wa viti maalumu katika Bunge kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 66, 78 na 81 ya Katiba. | Hakuna mfumo maalum ulioanzishwa na Tume kwa ajili ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za ubunge. | **Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke:**<br><br>112.-(1) - Kutakuwa na Wabunge wanawake wa viti maalumu katika Bunge kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 66, 78 na 81 ya Katiba ambapo **Tume itaweka mfumo mzuri wa utakaoelekeza kila chama kuteua wagombea wawili (ke na Me) katika kila jimbo la uchaguzi.** | **Hii itasaidia kufikia usawa wa jinsia na uwiano sawa wa kijinsi katika nafasi za ubunge.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu 113 **Uteuzi wa Madiwani Wanawake viti Maalum** | 113.-(1) Kutakuwa na viti maalumu vya wanawake katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji). | | 113.-(1) Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke: 113.-(1) - Kutakuwa na viti maalumu vya wanawake katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji). **ambapo Tume itaweka mfumo mzuri wa utakaelekeza kila chama kuteua wagombea wawili (Ke na Me) katika kila jimbo la uchaguzi.** | **Hii itasaidia kufikia usawa wa jinsia na uwiano sawa wa kijinsi katika nafasi za uongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.** |
| Kifungu cha 74 (3) **ufikiaji na matumizi ya vyombo vya habari** | 74.-(3) Kila chombo cha habari kinachomilikiwa na Serikali kinachochapisha taarifa kuhusu mchakato wa uchaguzi kitaongozwa na misingi ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi kwa namna kitakavyowatendea wagombea katika uandishi wa habari na kwa kiwango cha nafasi kitakachotengwa kwa ajili ya wagombea. | **Kifungu hiki hakijabainisha upendeleo na ubaguzi kwa misingi ya Kijinsia na rika.** | 74.-(3) Kila chombo cha habari **cha Umma** kinachochapisha taarifa kuhusu mchakato wa uchaguzi kitaongozwa na misingi ya kutokuwa na upendeleo na kuepuka ubaguzi **wowote ikiwemo wa Kijinsia, rika na watu wenye ulemavu** kwa namna kitakavyowatendea wagombea katika uandishi wa habari na kwa kiwango cha nafasi kitakachotengwa kwa ajili wagombea. | **Kuepuka upendeleo na ubaguzi wa Kijinsia na rika.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Saba Sehemu ya Kwanza (114- (1) hadi 136-i) **Makosa na adhabu** | | | 1. Adhabu ya faini katika kifungu 114 ni ndogo. Tunapendekeza adhabu ya faini kwa makossa yaliyoorodheshwa kuanzia Kif. 114 – 136 iwe kati ya TZS 500,000 – 1,000,000.<br>2. Nyaraka, vipeperushi na mabango kuwa na utambulisho wa mpiga chapa ni kwa nia gani?<br>3. Makosa yanayohusu ukatili wa jinsia wakati wa uchaguzi hayajabainishwa katika makos a na adhabu. | |
| Kifungu cha 6 (1); 6 (2); na 6 (3) **Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | 6 (1) - "Kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya Sheria hii, kila Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya atakuwa msimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata na msimamizi huyo wa uchaguzi anaweza kuwa msimamizi wa uchaguzi kwa jimbo zaidi ya moja" | a) Matumizi ya Wakurugenzi na Watumishi wa Umma kwenye uchaguzi kwa nafasi zao inaminya fursa kwa Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu kuwa Wasimamizi na Waratibu wa Uchaguzi.<br><br>b) Watumishi wa Umma waandamizi wenye uwezekano wa kuonekana na kuteuliwa wengi wao ni wanaume hivyo kuwanyima Wanawake na wasichana fursa ya kusimamia uchaguzi. | **Kifungu hiki kifutwe.**<br><br>**Kifungu hiki kifutwe.** | **Kina minya uwezekano wa Wanawake kusimamia Uchaguzi.**<br><br>**Kina minya uwezekano wa Wanawake kusimamia Uchaguzi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 6 (1); 6 (2); na 6 (3) **Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | 6 (2) - "Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyonayo mtu katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma wenye sifa sawa na za Mkurugenzi aliyerejewa katika kifungu kidogo cha (1), idadi ya wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata" | **Kama ilivyo hapo juu** | **Kama ilivyo hapo juu.** | **Kama ilivyo hapo juu.** |
| Kifungu cha 6 (1); 6 (2); na 6 (3) **Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | 6 (3) - Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2), Tume inaweza, pale ambapo mazingira yatahitaji na kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, kuteua mtu yeyote kutoka katika ofisi ya umma kwa jina au kwa nafasi yake kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi katika jimbo au kata yoyote badala ya yule aliyetajwa katika kifungu kidogo cha (1) na (2), na iwapo mtu huyo anateuliwa, Mkurugenzi wa Jiji, Mkurugenzi wa Manispaa, Mkurugenzi wa Mji, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya au afisa, kwa kadri itakavyokuwa, atakoma kuwa msimamizi wa uchaguzi au msimamizi msaidizi wa uchaguzi wa jimbo au kata hiyo katika uchaguzi huo. | | | |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Saba Kifungu cha 6 (4) **Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | 6 (4) - "Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria hii, Tume inaweza kumteua mtu yeyote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanayohusiana na mchakato wa uchaguzi" | Kifungu hiki hakijabainisha sifa za mtu kuteuliwa kuhudumu kama msimamizi wa uchaguzi au mtendaji wa tume, pia hakijabainisha utaratibu na namna ya uteuzi na pia hakijazingatia usawa wa Jinsia. | Kuwepo Kifungu Kipya cha 6 (1) kitakachosomeka: Kutakuwa na wasimamizi, waratibu, waandikishaji na watendaji wengine wa Tume ambao wataanzishwa na Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na ambao watakuwa na jukumu la kusimamia Uchaguzi ambao Mchakato wa uteuzi au ajira zao utafanywa kwa weledi na uwazi wa hali ya juu ili kupata watendaji ambao watajumuisha wanaume, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa uwiano mzuri. | **Mchakato wa Usimamizi wa Uchaguzi lazima uwe shirikishi na Jumuishi.** |
| Sura ya Saba Kifungu cha 6 (4) **Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | | | Kifungu 6 (2) kiandikwe upya na Kisomeke:<br><br>"Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria hii, Tume itateua au kuajiri watumishi na watendaji wenye sifa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume yanayohusiana na mchakato wa usimamizi wa uchaguzi kwa kuzingatia usawa wa Kijinsia'.<br><br>Kifungu kipya 6 (3) Kisomeke:<br>6 (3) - "Msimamizi wa uchaguzi au mtendaji wa Tume atateuliwa kwa kuzingatia sifa zifuatazo.<br><br>1. Awe raia wa Tanzania.<br>2. Mwaminifu na mwadilifu.<br>3. Uzoefu katika uchaguzi. | **Sifa na utaratibu wa kuwapata watendaji wa Uchaguzi lazima ziwekwe wazi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Saba<br>Kifungu cha 6 (4)<br>**Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | | | 4. Asiwe mwanachama wa au kufungamana na chama chochote cha siasa.<br>5. Awe na kiwango cha elimu. kisichopungua astashahada.<br>6. Asiwe na historia ya kutiwa hatiani kwa makosa ya jinai ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia na uaminifu.<br>7. Na sifa nyingine za ushindani katika soko la ajira. | **Sifa na utaratibu wa kuwapata watendaji wa Uchaguzi lazima ziwekwe wazi.** |
| Sura ya Saba<br>Kifungu cha 6 (4)<br>**Uteuzi wa wasimamizi wa uchaguzi na watendaji wengine** | | | **Kifungu Kipya cha 6 (4) kisomeke:**<br><br>6(4) - “utaratibu na namna ya uteuzi utakuwa kama ifuatavyo<br>1. Kutangazia umma nafasi za ajira ya wasimamizi wa uchaguzi.<br>2. Kuchuja na kusaili majina ya wenye sifa kwa kuzingatia Jinsi, rika, hali ya ulemavu mijini na vijijini.<br>3. Kuteua wenye sifa kulingana na mahitaji.<br>4. Kutangaza wateule katika gazeti la serikali. | **Sifa na utaratibu wa kuwapata watendaji wa Uchaguzi lazima ziwekwe wazi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 7(4) **Maafisa uandikishaji** | "Afisa mwandikishaji, kwa kuzingatia maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, anaweza kuteua idadi ya watendaji kama watakavyohitajika kwa madhumuni ya kuandikisha wapiga kura katika jimbo au kata". | Kifungu hiki kinampa mamlaka afisa mwandikishaji kuteua waandikishaji wasaidizi wa uchaguzi. | **Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke; 7(4) (a)**<br><br>**"Afisa mwandikishaji kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ataratibu upatikanaji wa waandikishaji wasaidizi watakaofanya kazi chini yake kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi na kwa kuzingatia usawa wa Jinsia na ujumuishaji wa makundi yote"** | **Kuepusha mianya ya rushwa na kuleta uwiano na usawa wa Jinsia.** |
| Kifungu cha 7(4) **Maafisa uandikishaji** | | | 7 (4) (b) Ili kuongeza ushiriki wa makundi yote katika uchaguzi, tume itaweka utaratibu kuwezesha walioko mahabusu, magereza, hospitalini na safarini kuweza kupiga kura.<br><br>7 (4) (c)Kwa ajili ya upigaji kura kwa watanzania walioko nje ya nchi, ubalozi wa Tanzania katika nchi husika utakuwa kituo cha uandikishaji wapiga kura, na kwamba,<br><br>Tume itateua mtu mwenye sifa kuwa afisa mwandikishaji wa wapiga kura katika kituo hicho. | **Ili kuongeza ushiriki wa makundi yote katika uchaguzi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 20 (2) na 21 (2)<br><br>**20(2)<br>Kupotea, kufutika au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura** | 20 (2) "...... atampa mwombaji kadi mpya ya mpiga kura baada ya mwombaji kulipa ada iliyoainishwa, ikiwa ipo, na iwapo maombi yatafanyika kutokana na kuharibika au kufutika kwa kadi ya mpiga kura, mwombaji atarudisha kadi hiyo iliyoharibika au iliyofutika | Vifungu hivi vinaweka gharama za malipo ya kitambulisho kilichopotea, kufutika au kuharibika au kubadilika kwa taarifa vinapunguza wigo wa wapiga kura na kuwanyima fursa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao wengi wao wana kipato kidogo. | 1. Kusiwe na gharama za kupata kitambulisho kipya cha mpiga kura.<br><br>2. Tunapendekeza maneno "ada" kufutwa.<br><br>3. Matumizi ya Vitambulisho mbadala yaruhusiwe kama vile NIDA, Leseni ya udereva na Hati ya Kusafiri. | **Ili kuhamasisha mwitikio wa wapiga kura na kuongeza wigo mpana wakushiriki uchaguzi kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele kijinsia.** |
| 21(2)<br>**Marekebisho ya taarifa** | 21(2)<br>"...kadi mpya ya mpiga kura haitatolewa chini ya kifungu hiki hadi mwombaji atakaporejesha kadi yake ya mpiga kura au atakapomthibitishia afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura kuwa kadi hiyo imepotea au imeharibika na amelipa ada iliyoainishwa..." | | **4. Kuwepo na vitambulisho maalum kwa kuzingatia watu wenye mahitaji maalum kama vile wasioona na viziwi.**<br><br>5. **Matumizi ya TEHAMA yawezeshe utambuzi wa mpiga kura hata pale ambapo kadi ya mpiga kura imepotea, kuharibika au kufutika.** | |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 85 (2)<br>**Kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupiga kura** | **"Mtu hataruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura isipokuwa wafuatao"** | 1. Kusahaulika kwa waandishi wa habari.<br><br>2. Afisa mwingine yoyote anayehusika na usalama kituoni ni tata na inaweza kutumika vibaya | Tunapendekeza neno mtu yeyote lifutwe.<br><br>Tunapendekeza kujumuishwa kwa waandishi wa habari kama sehemu ya watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupiga kura.<br>Hivyo kuongeza aya isomeke hivi 85 (2) (n) waandishi wa Habari. | **Kutoa fursa kwa watanzania kujua kinachoendelea ndani ya kituo.** |
| 85 (4)<br>**kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura** | **"Tume inaweza kualika watazamaji wa ndani na wa kimataifa na kuandaa mwongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji"** | Matumizi ya neno "inaweza" kwenye kifungu hiki inatoa hiari kwa tume kuwaalika au kutowaalika watazamaji wa uchaguzi.<br><br>Kuongeza aya kwenye kifungu hiki | **Kifungu 85 (4) kisomeke;**<br>"Tume itaalika na kusajili watazamaji wa ndani na wa kimataifa na kuandaa mwongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji."<br>85 (4) A.<br><br>Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki tume itashirikiana na makundi ya wananchi ikiwemo asasi za kiraia katika kuandaa muongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji wa uchaguzi. | **Kuepuka matumizi mabaya ya mamlaka.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 85 (2) **Kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupiga kura** | **“Mtu hataruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura isipokuwa wafuatao”** | 1. Kusahaulika kwa waandishi wa habari.<br><br>2. Afisa mwingine yoyote anayehusika na usalama kituoni ni tata na inaweza kutumika vibaya | Tunapendekeza neno mtu yeyote lifutwe.<br><br>Tunapendekeza kujumuishwa kwa waandishi wa habari kama sehemu ya watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura.<br>Hivyo kuongeza aya isomeke hivi 85 (2) (n) waandishi wa Habari. | **Kutoa fursa kwa watanzania kujua kinachoendelea ndani ya kituo.** |
| 85 (4) **kuruhusiwa kuingia katika kituo cha kupigia kura** | **“Tume inaweza kualika watazamaji wa ndani na wa kimataifa na kuandaa mwongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji”** | Matumizi ya neno “inaweza” kwenye kifungu hiki inatoa hiari kwa tume kuwaalika au kutowaalika watazamaji wa uchaguzi.<br><br>Kuongeza aya kwenye kifungu hiki | **Kifungu 85 (4) kisomeke;**<br>“Tume itaalika na kusajili watazamaji wa ndani na wa kimataifa na kuandaa mwongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji.”<br>85 (4) A.<br><br>Bila kuathiri masharti ya kifungu hiki tume itashirikiana na makundi ya wananchi ikiwemo asasi za kiraia katika kuandaa muongozo kwa ajili ya kusimamia mwenendo wa watazamaji wa uchaguzi. | **Kuepuka matumizi mabaya ya mamlaka.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# A. MUSWADA WA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2023.

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu kipya kuhusu **Ulinzi na Usalama wakati wa Uchaguzi** | **Hakuna kifungu mahsusi.** | Masuala ya Ulinzi na Usalama wakati wa Uchaguzi ni lazima yajitokeze bayana katika Sheria ili kudhibiti vitendo vya uvunjifu wa amani. | **Tunapendekeza kifungu kipya kitakachosomeka:**<br>169 (1) 'Kutakuwa na kikosi Maalum cha Polisi watakaofanya kazi ya kulinda amani na utulivu wakati wote wa Uchaguzi'.<br><br>169 (2) Tume itawapatia mafunzo Polisi wote wa Kikosi Cha Uchaguzi kuhusu masuala ya Michakato ya Uchaguzi ikiwemo unyanyasaji, udhalilishaji na ukatili Kijinsia.<br><br>169 (3) Polisi wa Kikosi Cha Uchaguzi watakula kiapo cha uaminifu na uadilifu mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo kabla ya kuanza majukumu ya Uchaguzi.<br><br>169 (4) Kikosi Cha Polisi Cha Uchaguzi kitaundwa kwa misingi ya uwiano wa Kijinsia | **Fujo na vurugu za uchaguzi zimekuwa tishio kwa Demokrasia ya Uchaguzi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sura ya Kwanza Kifungu cha 3: **Tafsiri ya dhana** | **Dhana za Jinsia** | Dhana za Jinsia hazikutafsiriwa. | **Uongezewe tafsiri za Jinsia:** **Jinsia:** ni tafsiri ya jamii kuhusu maana, stahiki na wajibu wa kuwa mwanamke au mwanaume kwenye jamii. Dhana hii imejengeka kwenye Imani zilizojikita au zinazoamini kwamba uongozi kwenye jamii zetu lazime upewe wanaume, na hivyo kuwapa haki na stahiki nyingi zinazoashiria kujenga tabaka kati ya wanaume na wanawake katika kufikia, kumiliki hata kunufaika na rasimali za jamii, | |
| Sura ya Kwanza Kifungu cha 3: **Tafsiri ya dhana** | | | **Jinsi:** Ni tofauti za kibalojia ambazo mtu anazaliwa kama me au ke, na tofauti kubwa licha ya maumbile tofauti ni kwenye kuendeleza kizazi.<br><br>**Usawa wa kijinsia:** ni mfumo wa maisha ambapo tofauti za kufikia na kunufaika na haki za binadamu haziko husussan katika umiliki wa mali, uongozi na katika shughuli ambazo hazitokani na tofauti za kimaumbile.<br><br>**Rushwa ya ngono:** ni aina ya rushwa inayohusisha matumizi mabaya ya mamlaka pale ambapo mtu mwenye mamlaka anatumia cheo chake kudai ngono ili ampe mhusika stahiki yake. Hii ni tofauti na biashara ya ngono pale ambapo watu wawili wanakubaliana kubadilisha ngono kwa ajili ya fedha au cheo. | |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 5(1) **Muundo wa Tume** | 5.-(1) Tume itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine watano watakaoteuliwa na Rais. | Kifungu cha 5 (1) hakijazingatia usawa wa Jinsia katika uteuzi wa tume. | Kifungu hiki kirekebishwe ili msingi wa usawa wa jinsia uingizwe na kisomeke: 5 (1) - 'Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu wake pamoja na Wajumbe **utazingatia usawa wa Jinsia'.** | Hii itasaidia katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi za juu za maamuzi ya Tume ya Uchaguzi. |
| Kifungu 5 (3)<br><br>**Muundo wa Tume** | 5 (3) - Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume utafanywa kwa misingi kwamba, endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. | Kifungu hakijazingatia uwiano wa Jinsi. | 5 (3) - Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume utafanywa kwa misingi kwamba, endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano **na kwamba endapo Mwenyekiti atakuwa Mwanamke, Makamu Mwenyekiti atakuwa Mwanaume.** | **Kuleta uwiano wa Jinsi katika ngazi ya Juu ya maamuzi ya Tume.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 8 (2) (e) (ii)<br><br>**Muda wa Utumishi wa Wajumbe** | 8 (2) (e) ikiwa ataondolewa madarakani na Rais kutokana na-<br><br>(i) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya maradhi au sababu nyingine yoyote;<br>**(ii) tabia mbaya; au**<br>(iii) Kupoteza sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe. | Neno tabia mbaya linazua utata. | Kifungu 8 (2) (e) kisomeke:<br><br>**'...kukiuka maadili ya kanuni za uongozi na utumishi wa Tume'** | **Kuondoa utata wa neno tabia mbaya.** |
| Kifungu cha 8 –<br><br>**Kamati ya Uchunguzi (4)** | 8 (4) - Kamati iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) itajumuisha wajumbe wafuatao:<br><br>(a) Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br><br>(b) Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; | Kifungu hiki hakijazingatia uwiano wa Jinsia. | 8 (4) - Kamati iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) Itazingatia usawa wa jinsia na itajumuisha wajumbe wafuatao:<br>(a) Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br><br>(b) Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.<br><br>(c) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; | **Ili kuongeza uwiano wa Jinsia kwenye Kamati ya Uchunguzi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 8 –<br><br>**Kamati ya Uchunguzi (4)** | (c) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;<br><br>(d) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar;<br><br>(e) wajumbe wawili wenye uzoefu wa masuala ya uchaguzi, mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar; na<br><br>(f) Mjumbe mmoja kadri Rais atakavyoona inafaa kwa kuzingatia jinsia. | Kifungu hiki hakijazingatia uwiano wa Jinsia. | 8 (4) - Kamati iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (3) Itazingatia usawa wa jinsia na itajumuisha wajumbe wafuatao:<br>(a) Jaji wa Mahakama ya Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br><br>(b) Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.<br><br>(c) Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;<br><br>(d) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar.<br><br>(e) wajumbe wawili wenye uzoefu wa masuala ya uchaguzi, mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar kwa msingi **kuwa mmoja atakuwa Mwanamke; na**<br><br>(f) Mjumbe mmoja kadri Rais atakavyoona inafaa kwa kuzingatia jinsia. | **Ili kuongeza uwiano wa Jinsia kwenye Kamati ya Uchunguzi.**<br><br>**Ili kuongeza uwiano wa Jinsia kwenye Kamati ya Uchunguzi.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 9 (1)<br><br>**Kamati ya Usaili** | 9.-(1) Wakati wowote inapobidi kuteuliwa mjumbe au wajumbe wa Tume, Kamati ya Usaili itaitishwa.<br>(2) Kamati itakayoitishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa na wajumbe wafuatao:<br><br>(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;<br><br>b) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;<br><br>c) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na<br><br>d) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kwa kuzingatia jinsia. | Kifungu hiki hakijazingatia uwiano wa Jinsia. | 9 (1) –Wakati wowote inapobidi kuteuliwa mjumbe au wajumbe wa Tume, Kamati ya Usaili itaitishwa. (2) Kamati itakayoitishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) Itakuwa na wajumbe wafuatao:<br>a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;<br><br>b) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;<br><br>c) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na<br><br>d) Mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kwa kuzingatia jinsia. | **Kuleta uwiano wa Jinsia kwenye Kamati ya Usaili.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 9 (2)<br><br>**Kamati ya Usaili** | Kamati itakayoitishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa na wajumbe wafuatao:<br><br>(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;<br><br>(b) Jaji Mkuu wa Zanzibar ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;<br><br>(c) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na<br><br>(d) mjumbe mmoja atakayeteuliwa na Rais kwa kuzingatia jinsia.<br><br>(3) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa katibu wa Kamati ya Usaili.<br><br>(4) Wajumbe wa Kamati ya Usaili wataapa mbele ya Rais kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yao. | Kifungu hiki kinawaweka wateule wa Rais kuwa wajumbe wa Tume hii kwa sehemu kubwa itasababisha kuwa na ushiriki hafifu wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwani nafasi hizo kwa sehemu kubwa zinashikiliwa na wanaume. Kifungu hiki hakijazingatia usawa wa jinsia katika vigezo vya kuteua wajumbe. | Tunapendekeza kufungu hiki kisomeke hivi:<br><br>Wajumbe wa kamati ya Usaili watateuliwa kutoka katika vyama vya wanasheria, Sekretarieti ya utumishi wa Umma, makundi ya jamii kwa kuzingatia uwiano na usawa wa jinsia. | |

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 9 (2)<br><br>**Kamati ya Usaili** | (5) Ndani ya siku kumi na nne baada ya kuundwa, Kamati ya Usaili itatoa tangazo kwa umma kupitia magazeti angalau mawili yenye wigo mpana wa usambazwaji nchini na vyombo vingine vya habari kuwaalika wananchi wenye nia ya kuomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume kuwasilisha maombi yao kwenye Kamati.<br><br>(6) Kamati ya Usaili mara baada ya kupokea na kuchambua maombi ya watu walioomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume, itafanya usaili na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume.<br><br>(7) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (6), utaratibuwa kusimamia mchakato wa usaili utakuwa kama utakavyoainishwa katika Kanuni.<br><br>(8) Kamati ya Usaili itawasilisha kwa Rais majina manne zaidi ya idadi ya nafasi zinazohitajika kujazwa.<br><br>(9) Muda wa Kamati ya Usaili utakoma mara baada ya raisi kuteua wajumbe wa Tume | | | |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Kifungu cha 9 (2)<br><br>**Kamati ya Usaili** | 9 (6) Kamati ya Usaili mara baada ya kupokea na kuchambua maombi ya watu walioomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume, itafanya usaili na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume. | Sharti la kuzingatia usawa wa jinsia katika kifungu hiki halijawekwa hivyo kuna uwezekano wa makundi ya wanawake, vijana na wenye ulemavu kusahaulika au kuwa na ushiriki mdogo. | 9 (6) Tunapendekeza kifungu hiki kisomeke hivi:<br><br>Kamati ya Usaili mara baada ya kupokea na kuchambua maombi ya watu walioomba kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume, itafanya usaili na kupendekeza kwa Rais majina ya watu wenye sifa za kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume kwa ***kuzingatia usawa wa jinsia na ujumuishi wa vijana na watu wenye ulemavu.*** | **Itasaidia kuwa na usawa wa jinsia katika ngazi za juu za maamuzi za uchaguzi kupitia tume ya Uchaguzi.** |
| Kifungu cha 18 - **Mkurugenzi wa Uchaguzi** | 18.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume. | Kifungu hiki hakizingatii misingi ya utawala bora | Kifungu cha 18.- (1) Kisomeke: 'Kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume **kwa kuzingatia mchakato wa usaili'.** | **Ili kuendana na misingi ya utawala bora.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# B. MUSWADA WA SHERIA YA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sehemu ya Tano:<br><br>**Masharti Mengineyo** | 27. Tume inaweza kutengeneza kanuni na miongozo na kutoa maelekezo kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. | | 27. Tume itatengeneza kanuni na miongozo yenye kuzingatia na kukidhi usawa wa Jinsia na kutoa maelekezo kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake. | **Ili kuendana na misingi ya utawala bora.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# C. MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASUALA YA VYAMA VYA SIASA, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| **Kifungu cha 13 kutaka kurekebisha Kifungu cha 10C (2)** | Sera ya Jinsia na Ujumuishi ya Vyama vya Siasa iliyorejewa chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa masuala yote yaliyobainishwa katika (JEDWALI LA TATU) | Kifungu hiki ni kizuri lakini kinakosa baadhi ya masuala muhimu ya usawa wa jinsia na ujumuishi wa vijana na watu wenye ulemavu. | Tunapendekeza vipengele viongezwe katika Jedwali la Tatu (THIRD SCHEDULE)<br><br>1. Utaratibu Chama cha siasa kitakachoweka ili kushughulikia makosa ya ukatili wa jinsia ikiwemo ukatili wa kingono ndani na nje ya vyama vya siasa.<br><br>2. Uwiano wa majina ya wagombea wanaopitishwa na vyama uzingatie kwenda Tume ya Uchaguzi jinsi yaani 50/50 kati ya wanawake na wanaume. Asilimia hizo zijumuishe vijana na watu wenye ulemavu.<br><br>3. Kuweka katazo kwa mgombea yeyote wa nafasi yoyote ya uongozi ndani na nje ya chama ambaye amethibitika kuwa ametenda vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwemo rushwa ya ngono.<br><br>4. Sheria ielekeze Baraza la Vyama vya Siasa kuwa na uwiano sawa wa wajumbe kati ya wanawake na wanaume katika Baraza la Vyama vya Siasa. Yaani 50/50 | **Kuongeza ushiriki wa wanawake na makundi maalum kushiriki katika ngazi za maauzi na uongozi katika vyama vya siasa.** |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# C. MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASUALA YA VYAMA VYA SIASA, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| Sehemu ya Tatu Kifungu cha 9 (10C) kinahusu **umuhimu wa kuwa na Sera ya Jinsia.** | Kifungu hiki ni cha nyongeza kinachovitaka vyama vya siasa kuwa na nakala mbalimbali mojawapo ikiwa Sera ya Jinsia. | | Kifungu hiki kibakizwe kilivyo kwani kinaimarisha utekelezwaji wa msingi wa usawa uliobainishwa katika Sheria ya 2018. 6A.-<br><br>(1) kinachowajibisha vyama vya siasa kuzingatia misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Zanzibar, usawa wa jinsia na jumuishi wa makundi yote.<br><br>(2) Pamoja na kuwajibika kuzingatia misingi ya demokrasia, utawala bora, kutoku bagua na usawa wa jinsia na jumuishi wa makundi yote. | **Kifungu hiki kitaimarisha utekelezaji wa misingi ya usawa wa jinsia na ujumuishi katika vyama vya siasa.** |
| | **Sehemu hii ya Tatu kifungu cha 11, Kuhusu Masharti ya maandamano.** | kimependekeza masharti ya maandamano ya vyama vya siasa kwa kuzingatia Sheria ya Polisi na huduma saidizi. Hata hivyo kifungu hiki hakitoi mapendekezo ya kuwalinda wanawake hususani wakati wa uchaguzi kutokana na fujo au ghasia zitokanazo na utekelezwaji wa jukumu hili wakati polisi wakizuia maandamano yanayoonekana au kuaashiria ukiukwaji wa masharti yaliyo bainishwa. | Kifungu hiki cha 11, kiongezewe kifungu kidogo (11 b) kitakachowajibisha Jeshi la polisi kulinda wanawake kutokana na vitendo vitakavyaashiria kuwaumiza wakati jeshi hili likizuia maandamano yanayoonekana kwamba siyo halali. | Kuimarisha ulinzi na usalama wa wanawake na watu wenye ulemavu wakati wa uchaguzi, hii itaongeza wigo wa ushiriki katika uchaguzi. |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# C. MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASUALA YA VYAMA VYA SIASA, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| | **Sehemu ya Tatu Kifungu cha 16 Kuhusu mgawanyo wa ruzuku** | Kifungu hiki kinabainisha au kutoa mwongozo kuhusu mgawanyo wa ruzuku za vyama vya siasa lakini kiko kimya kuhusu matumizi ya ruzuku kwa ajili ya kuwezesha utekelezwaji wa Kifungu cha Nyongeza cha 10C, kinachovitaka vyama vya siasa viwe na sera ya jinsia yenye kubainisha program za jinsia, program za uwezeshwaji wa wanawake pamoja na kuwa na vitengo vya jinsia vya kusimamia utekelezwaji wa program hizo. | Kifungu hiki kifanyiwe marekebisho ili kuwajibisha vyama kutumia ruzuku kwa ajili ya kutekeleza matakwa ya kifungu cha nyongeza cha 9 (10C). | **Kitasaidia katika kuweka mipango na bajeti/ mgawanyo wa ruzuku na rasilimali za vyama vya siasa kwa mrengo wa jinsia.** |
| | **Kifungu cha Pili: kuhusu gharama za uchaguzi Sura 278 kifungu cha 7** | Kifungu hiki hakiwajibishi vyama vya Siasa kuhakikisha gharama za uchaguzi zinatumika katika kutekeleza Kifungu cha nyongeza cha 9(10c) | Kifungu cha nyongeza kiwekwe kitakacho semeka: Vyama vya siasa viwajibike kutenga fungu maalum kuwezesha utekelezwaji wa kifungu cha nyongeza cha 9 (10c) kutekeleza sera ya jinsia iliyobainishwa katika kifungu hiki cha nyongeza | Kuhakikisha vyama vinawajibika kutenga rasilimali za utekelezaji wa Sera ya Jinsia katika vyama |

JEDWALI LA MAONI KWENYE VIFUNGU VYA MISWADA

# C. MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASUALA YA VYAMA VYA SIASA, 2023

| KIFUNGU | MAUDHUI YA KIFUNGU | MAPUNGUFU | MAPENDEKEZO | SABABU ZA MAPENDEKEZO |
|---|---|---|---|---|
| | Sehemu ya Tatu Kifungu cha 9 (10C). Kifungu hiki ni cha nyongeza kinachovitaka vyama vya siasa kuwa na Sera ya Jinsia itakayobaini program za Jinsia, mikakati ya kuwezesha wanawake, na kuwa na dawati la jinsia la kuratibu utekelezwaji wa Sera ya Jinsia | Kifungu hiki kibaki lakini kiongeze kifungu kidogo cha kuwajibisha vyama vya siasa kuweka mikakati ya ufuatiliji wa sera hii na mipango yake | Kifungu hiki cha 10C kiongezewe kipengele cha ziada kitaka cho someka : Vyama vya siasa viwajibike kwenye kutenga fungu la kuwezesha utekelezwaji wa sera hii ya jinsia. | **Kuhakikisha vyama vinawajibika kutenga rasilimali za utekelezaji wa misingi ya Sera ya Jinsia katika vyama.** |
| | **Sehemu ya Tatu Mabadiliko ya Kifungu cha 6A** | KifunKifungu hiki hakikubaini mwongozo wa kuzingatia misingi ya usawa kama ilivyotajwa kwenye kifungu cha 6A katika sheria ya vyama vya siasa ya 2018. | Kifungu hiki kiongezewe kifungu kidogo kitakacho someka: Vyama vya siasa viwajibike kuzingatia utekelezwaji wa msingi huu na kuwania viti vya uwakilishi kwenye chaguzi za ndani ya vyama na chaguzi za kitaifa. Lengo ni kufikia 50/50 kwenye uteuzi wa wanawake kwenye uongozi wa vyama. | Kuwajibisha vyama kuwa na ushiriki wa wanawake katika uongozi na maamuzi kwa 50/50. |

TGNP

MTANDAO WA JINSIA
TANZANIA